

# HAKI MAHAKAMANI

## Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.

TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA  
(DESIGN AND DRAWING)  
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA  
NA ROYAL DANISH EMBASSY  
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT  
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)



IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA  
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

## **HAKI ZA MTUHUMIWA/MSHITAKIWA MAHAKAMANI**

1. Mtu yeyote anayeshitakiwa na kosa la jinai ana haki kutendewa kama mtu asiye na kosa hilo mpaka itakapothibitishwa kuwa anayo hatia.
2. Mtuhumiwa/Mshitakiwa anayo haki ya kuomba dhamana isipokuwa pale sheria inapokataza. Ikiwa maombi yake hayatakubalika anaweza kupeleka maombi yake katika mahakama za juu.
3. Mshitakiwa anaposomewa shitaka ana haki ya kufahamishwa na kufafanuliwa shitaka linalomkabili ili kulielewa.
4. (a) Ikiwa mshitakiwa atakataa shitaka itabidi upande wa mashitaka kuleta mashahidi (ushahidi mahakamani kuthibitisha shitaka).  
  
(b) Ikiwa mshitakiwa atakubali shitaka, maelezo ya shitaka yatatolewa na upande wa mashtaka. Mshitakiwa anayo haki ya kukubali au kukataa usahihi wa maelezo hayo yatakayotolewa.  
  
(c) Ikiwa mshitakiwa atakataa maelezo ya shitaka/ kosa, upande wa mashitaka itabidi ilete mashahidi ushahidi kuthibitisha shitaka.  
  
(d) Ikiwa mshitakiwa atakubali usahihi wa maelezo ya kosa/mashtaka, hakimu atamtia hatiani. Mshitakiwa atapewa fursa ya kutoa maelezo yake ya mwisho, utetezi (allocatus) kabla ya adhabu kutolewa.

5. Mshitakiwa anayo haki ya utetezi na kuwa na wakili.
6. Mshitakiwa anayo haki ya kuwepo mahakamani wakati wa uendeshaji wa kesi yake.
7. Mshitakiwa anaweza akaomba ufafanuzi wa maelezo yanayotolewa mahakamani.
8. Mshitakiwa anayo haki ya kuwauliza maswali mashahidi wa upande wa mashitaka pindi wamalizapo kutoa ushahidi.
9. Baada ya upande wa mashitaka kumaliza ushahidi, mshitakiwa anaweza akaiomba mahakama ifutilie mbali kesi ikiwa anaona ushahidi haukumhusisha na kosa linalomkabili (plea of No case to answer).
10. (a) Mshitakiwa anayo haki ya kuelezwa kama ana kesi ya kujibu au ya baada ya upande wa mashitaka kukamilisha ushahidi wake.  
  
(b) Ikiwa mshitakiwa atakuwa na kesi ya kujibu ni budi hakimu amjulishe kuwa anaweza kutoa ushahidi wake kwa kiapo au bila kiapo, na pia kwamba ana haki ya kuita mashahidi kama anao.  
  
(c) Mshitakiwa anapaswa kuelezwa kuwa anaweza kukaa kimya bila kutoa utetezi wake lakini kufanya hivyo kunaweza kukaifanya mahakama ichukulie kuwa yale yaliyosemwa na upande wa mashtaka ni kweli na hivyo kumtia hatiani (The court can draw adverse inference on his silence).

11. Mshitakiwa anaweza kuulizwa maswali mara ama lizapo utetezi wake.
12. Mshitakiwa ana haki ya kutoa maelezo ya mwisho kuhusu mwenendo mzima wa kesi.
13. Mshitakiwa anayo haki ya kuiomba mahakama kumwita shahidi wa upande wa mashitaka ambaye hakuitwa au ambaye tayari ameitwa ili kutoa ushahidi tena.
14. Mshitakiwa anayo haki ya kuwepo mahakamani hukumu inaposomwa.
15. Mshitakiwa anayo haki ya kukata rufaa kwenye mahakama ya juu katika siku zilizopangwa kisheria kama atakuwa hajaridhika na hukumu, au adhabu pekee iliyotolewa na mahakama.
16. Mshitakiwa anayo haki ya kupewa nakala ya mwenendo wa kesi na hukumu ikiwa atatoa taarifa ya nia ya kutaka kuomba rufaa.
17. Mshitakiwa anayo haki ya kuomba dhamana wakati akisubiri rufaa dhidi ya kutiwa hatiani na kifungo au kifungo pekee.